**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

TANZANIA
COOPERATIVE DEVELOPMENT COMMISSION
Together We Build Our Economy

# *MWONGOZO WA UTOAJI ELIMU NA MAFUNZO KWA VYAMA VYA USHIRIKA*


***IMEANDALIWA NA:***
TUME YA MAENDELEO YA
USHIRIKA S. L. P 201,
DODOMA.



**JULAI 2021** **TOLEO LA KWANZA**

## YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
SEHEMU YA PILI ........ 2
2.1. UMUHIMU WA ELIMU NA MAFUNZO ........ 3
SEHEMU YA TATU ........ 4
3.0 WATUMIAJI WA MWONGOZO ........ 4
3.1 WAPOKEAJI WA ELIMU NA MAFUNZO ........ 4
3.2 WATOAJI WA ELIMU NA MAFUNZO ........ 4
SEHEMU YA NNE ........ 5
4.0 MAMBO YA KUZINGATIA KABLA NA BAADA YA KUTOA ELIMU ........ 5
4.1 KABLA YA KUTOA MAFUNZO ........ 5
4.2 BAADA YA KUTOA MAFUNZO ........ 6
SEHEMU YA TANO ........ 7
5.0 GHARAMA ZA ELIMU NA MAFUNZO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA ........ 7
SEHEMU YA SITA ........ 7
6.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA KUTOA ELIMU NA MAFUNZO ........ 7
6.1 Majukumu ya TUME ........ 8
6.2 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) ........ 9
6.3 Majukumu ya Wadau wengine (TFC & SCCULT) ........ 10
6.4 Vyama vya Ushirika ........ 10
SEHEMU YA SABA ........ 11
7.0 UTOAJI WA ELIMU NA MAFUNZO ........ 11
7.1 Kamati ya Kitaifa ya Elimu na Mafunzo ........ 11
7.2 Majukumu ya Kamati ya Kitaifa ya Elimu na Mafunzo ........ 12
7.3 Kamati za Elimu na Mafunzo ya Ushirika za Mikoa ........ 12
7.3.1 Wajumbe wa Kamati za Mikoa ........ 13
7.3.2 Majukumu ya Kamati za Mikoa ........ 13
SEHEMU YA NANE ........ 14

8.0 MBINU ZA KUTOA ELIMU NA MAFUNZO ........ 14

SEHEMU YA TISA ........ 15

9.0 UFUATILIAJI, TATHMINI NA URATIBU ........ 15

10.0 HITIMISHO ........ 15


## DIBAJI

**Chimbuko la Mwongozo wa Elimu na Mafunzo.**

Kutokana na Ushirika kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mabadiliko ya mazingira hasa ukuaji wa sayansi na teknolajia, utandawazi, ushindani na soko huru, jitihada za makusudi lazima zichukuliwe ili kuvinusuru Vyama vya Ushirika kutoka katika hali hii. Pande zote zinazohusika katika Ushirika hazina budi kuwa na taarifa sahihi, upashanaji wa habari, elimu na mafunzo sahihi juu ya nini ushirika unawataka wafanye. Elimu na mafunzo sahihi ni nyenzo pekee itakayotumika katika kuvijenga Vyama vya Ushirika imara, endelevu, vinavyojibu mahitaji ya wanachama na kutoa matokeo tarajiwa. Aidha, kundi kubwa la wanaushirika linaloundwa na pembetatu ya ushirika yaani, **Wanachama, Viongozi, na Watendaji.** Kwa muda mrefu sasa halina elimu na mafunzo sahihi ya Ushirika. Kwa kuzingatia dhamana kubwa waliyonayo Wanachama, Viongozi na Watendaji katika kujenga Ushirika imara na endelevu, ni dhahiri udhaifu unaoonekana katika Ushirika unasababishwa na ukosefu wa elimu na mafunzo sahihi kwa kundi hili adimu la elimu ya Ushirika. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la watu, taasisi mbalimbali na kampuni binafsi (consultancy firms) zinazojishughulisha na utoaji wa elimu na mafunzo ya Ushirika kwa wanachama, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika, bila kuwa na mwongozo stahiki na uelewa wa kutosha juu ya dhana ya Ushirika. Kukosekana kwa mwongozo wa utoaji elimu na mafunzo ya ushirika kumesababisha kila anayetoa elimu na mafunzo ya Ushirika kutumia utashi wake na hatimaye kujenga uelewa tofauti kwa wanachama, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika. Hali hii imeathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Vyama vya Ushirika kwani kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Kanuni za Vyama vya Ushirika, na taratibu za Ushirika.

Sera ya Maendeleo ya Ushirika imefafanua umuhimu wa Elimu na Mafunzo sahihi kwa Wanachama, Wajumbe wa Bodi na Watendaji. Kwa muktadha huu, Tume ya Maendeleo ya Ushirika ikishirikiana na MUCCoBS, COASCO na TFC imeandaa mwongozo huu wa utoaji elimu na mafunzo sahihi kwa wanachama, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika. Lengo la mwongozo huu ni kujenga uelewa wa pamoja miongoni mwa watoa elimu na mafunzo ya Ushirika sanjari na kuwa na rejea ya kudumu pindi elimu na mafunzo yatakapokuwa yakitolewa. Mwongozo unajielekeza katika kutoa elimu na mafunzo sahihi kwa wanachama, viongozi na watendaji ili kujenga Ushirika unaokwenda na wakati na unaojibu mahitaji ya wanachama wake.

Ikumbukwe kuwa elimu na mafunzo ya Ushirika ni tasnia pana sana, na isingewezekana kujumuisha kila kitu katika mwongozo huu. Hivyo, watoa elimu lazima wajijengee uwezo juu ya falsafa ya Ushirika kwa kusoma maandiko mbalimbali yanayohusu Ushirika, Sera, Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali za Ushirika, na watoe elimu na mafunzo kwa wanachama, viongozi na watendaji kwa kuzingatia mwongozo huu.



Dkt. Benson O. Ndiege

**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA**

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 inaelekeza kuwa Elimu na Mafunzo ya ushirika ni moja ya misingi ya ushirika inayokusudia kuboresha uelewa na ujuzi kwa wanachama, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha, imefafanua umuhimu wa elimu na mafunzo sahihi kwa Vyama vya Ushirika ili kufikiwa kwa Dira ya mfumo wa Vyama vya Ushirika imara na endelevu na vyenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya wanachama ya kiuchumi na kijamii.

Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 pamoja na mambo mengine imeipa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania mamlaka ya kusimamia, kuratibu na kutoa mafunzo kwa Vyama vya Ushirika. Hivyo, imetoa mwanya kwa wadau kutoa mafunzo na imeelekeza kila chama cha ushirika kushiriki na kuwezesha suala la utoaji wa elimu na mafunzo kwa Wanachama wake, Wajumbe wa Bodi na Watendaji ili waweze kuwajibika ipasavyo na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya chama.

Elimu na mafunzo ya ushirika ni muhimu katika Sekta ya Ushirika; hivyo, Vyama vya ushirika vinatakiwa kutoa Elimu sahihi kwa wanachama, viongozi, watendaji na jamii kwa ujumla. Wadau wanaoshughulika na kutoa elimu katika sekta ya ushirika wanapaswa kuwa na weledi na upeo wa kutosha ili waweze kushindana katika soko kwa kuzingatia ubora wa huduma itolewayo kwa wakati sahihi ili kukidhi mahitaji ya wanachama na jamii kwa ujumla.

Hata hivyo, kumekuwepo na utaratibu usioridhisha wa utoaji elimu kwa Vyama vya Ushirika unaofanywa na watu binafsi na Taasisi mbalimbali. Utaratibu huo umesababisha kila anayetoa elimu na mafunzo ya Ushirika kutumia utashi wake na hatimaye kujenga uelewa tofauti kwa washiriki na jamii kwa ujumla. Hali hii imeathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Vyama vya Ushirika.

Kutokana na changamoto hii, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa mwongozo kwa kuainisha utaratibu wa namna bora ya utoaji wa elimu na mafunzo katika Vyama vya Ushirika Nchini. Mwongozo huu ukitumiwa ipasavyo utasaidia watoa elimu na mafunzo kwa Vyama Vya Ushirika ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya kiushirika kutegemeana na mahitaji ya Vyama.

Sheria ya Vyama Vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na Kanuni ya 81(1)(b) ya Kanuni za Vyama Vya Ushirika za mwaka 2015 zinampa mamlaka Mrajis ya kuandaa na kutoa miongozo na maelekezo yanayopaswa kuzingatiwa na Vyama vya Ushirika kwa ajili ya ustawi wa sekta ya Ushirika.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 LENGO LA MWONGOZO NA UMUHIMU WA ELIMU NA MAFUNZO

### 2.1 LENGO LA MWONGOZO

Mwongozo huu utasaidia Vyama vya Ushirika pamoja na Wadau wa Maendeleo ya Ushirika kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake wakati wa kutoa elimu kwa ajili ya ustawi wa vyama na

sekta nzima ya Ushirika. Vilevile, mwongozo huu utasaidia utoaji wa elimu inayofanana kwa walengwa na kuwa chachu ya Vyama vya Ushirika imara na endelevu badala ya kuendelea kuwa nadharia inayokinzana na isiyotekelezeka. Aidha, katika kufikia lengo hili mambo yafuatayo yatazingatiwa: -

- Namna bora ya utoaji wa elimu na mafunzo katika Vyama vya Ushirika. Utaratibu huo umebainisha kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kama msimamizi na mratibu wa wadau mbalimbali wa maendeleo ya Ushirika;
- Kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini aina ya mafunzo yanayohitajika kwenye Vyama vya Ushirika;
- Utayarishaji wa mpango wa mafunzo;
- Kuratibu ugharamiaji wa elimu na mafunzo ili kupunguza gharama kwa Vyama vya Ushirika na Wadau wa maendeleo ya Ushirika; na
- Kutambua sifa na uwezo wa watoaji wa mafunzo na kupata taarifa za mafunzo yanayotolewa kwenye Vyama vya Ushirika.

## 2.1. UMUHIMU WA ELIMU NA MAFUNZO

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu inayotumika katika kuvijengea uwezo Vyama vya Ushirika ili viwe imara na endelevu. Umuhimu wa elimu na mafunzo ni pamoja na:

i. Kuwawezesha wanachama, wajumbe wa Bodi na watendaji kutambua haki na wajibu wao;
ii. Kuelewa mazingira ya chama chao, shughuli za chama na kushiriki kikamilifu katika kuendesha shughuli za chama na kufikia malengo ya chama;

iii. Kusaidia kuongeza ufahamu wa wanachama na ujuzi kwa watendaji katika kuongeza ufanisi wa kazi kwa maendeleo ya chama.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 WATUMIAJI WA MWONGOZO

Elimu ya Ushirika ni muhimu katika maendeleo ya vyama vya ushirika na inapaswa kutolewa na wataalam wenye weledi kwa ngazi tofauti kulingana na mahitaji ya walengwa kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake, masharti ya chama pamoja na miongozo mbalimbali.Watumiaji wa Mwongozo huu wamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni wapokeaji na watoaji wa elimu na mafunzo.

### 3.1 WAPOKEAJI WA ELIMU NA MAFUNZO

i. Wanachama ;
ii. Wajumbe wa Bodi;
iii. Watendaji;
iv. Maafisa Ushirika; na
v. Jamii kwa ujumla.

### 3.2 WATOAJI WA ELIMU NA MAFUNZO

i. Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC);
ii. Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU);
iii. Shirika la Ukaguzi na Usimmizi wa Vyama Vya Ushirika (COASCO);
iv. Wizara za kisekta;
v. Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC na SCCULT);

vi. Wadau wengine watakaoidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAMBO YA KUZINGATIA KABLA NA BAADA YA KUTOA ELIMU

Ufanisi wa elimu na mafunzo katika Vyama vya Ushirika pamoja na mambo mengine unategemea umahiri wa wakufunzi ambao wana utaalamu na uzoefu wa kutosha katika mchepuo mahususi wa Ushirika. Ili kufikia azma hii Tume imeweka utaratibu ambao utapaswa kufuatwa kabla na baada ya kutoa elimu na mafunzo kama ifuatavyo:

### 4.1 KABLA YA KUTOA MAFUNZO

Mwezeshaji kabla ya kuanza kutoa elimu anapaswa kufanya yafuatayo:

**i) Upembuzi yakinifu wa mahitaji ya mafunzo**

Kufahamu ni wanachama wa aina gani anaolenga kuwafikia. Zoezi hili litafanyika kwa kufanya upembuzi wa mahitaji ya mafunzo (Training Needs Assessment) ili kujua anachotakiwa kuandaa.

**ii) Kuandaa Mpango kazi**

Mwezeshaji ataandaa mpango kazi ambao utaonesha kazi zitakazopaswa kufanyika kabla ya kutoa elimu na mafunzo ikiwa ni pamoja na mada zitakazowasilishwa ili kukidhi mahitaji ya walengwa. Mpango kazi huo utapaswa kuwasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya mapitio na kutoa ushauri.

**Kuhakiki mada**

Mada zilizoandaliwa zitapaswa kuwasilishwa katika ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika ili zihakikiwe Kwa lengo la kuhakikisha kuwa mada hizo zinakidhi viwango na mahitaji ya walengwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika iliyopo Pamoja na Kanuni zake na miongozo mbalimbali inayotolewa na Mrajis.

**iii) Kuainisha gharama za mafunzo**

Mwezeshaji anatakiwa kuainisha makadirio ya gharama (bajeti) za mafunzo hayo na watakaohusika kuchangia gharama hizo pale itakapo hitajika.

## 4.2 BAADA YA KUTOA MAFUNZO

Ili kuhakikisha kuwa elimu iliyotolewa inakuwa na manufaa kwa walengwa ni muhimu Mtoa elimu na mafunzo kutekeleza yafuatayo:

i) Kuandaa taarifa ya mafunzo na kuwasilisha katika Ofisi ya Mrajis;

ii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ili kupima ufanisi wa elimu na mafunzo aliyoyatoa.

iii) Kufanya tathmini nyingine kwa kuvitembelea vyama kwenye maeneo yao ili kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo waliyopata yanafanyiwa kazi katika uendeshaji wa shughuli za chama. Tathmini hii itasaidia kufanya maboresho katika mafunzo yatakayofuata; na

iv) Kuandaa taarifa ya tathmini ya mafunzo na kuiwasilisha kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya maamuzi na maelekezo.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 GHARAMA ZA ELIMU NA MAFUNZO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Kutokana na umuhimu wa elimu na mafunzo katika Vyama vya Ushirika kama ambavyo imeelekezwa na Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na Kanuni zake, vyama vyote vya ushirika vitatakiwa kutenga tengo la Elimu na Mafunzo na kuhakikisha kuwa mafunzo yanatolewa kulingana na mahitaji ya chama.

Baada ya fedha za elimu kutengwa inasisitizwa kuwa kipaumbele katika kugharamia mafunzo kiwekwe kwa wanachama ikifuatiwa na viongozi na watendaji wa chama. Elimu na Mafunzo pia yanaweza kugharamiwa na wafadhili na wadau mbalimbali wa maendeleo ya ushirika.

Ili kudhibiti gharama za elimu na mafunzo kwenye vyama vya ushirika, Mrajis atatoa waraka kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kuzuia watoa huduma kujipangia gharama kubwa za mafunzo zisizokuwa na tija kwenye vyama.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA KUTOA ELIMU NA MAFUNZO

Ili kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinakuwa imara na endelevu, wadau wa ushirika wameainishwa katika Sheria ya Vyama vya Ushirika kushiriki katika kuendeleza sekta ya ushirika. Majukumu ya wadau hao ni kama ifuatavyo:

## 6.1 Majukumu ya TUME

Majukumu ya Tume katika utoaji wa elimu na mafunzo ni pamoja na:

a) Kutoa mafunzo elekezi ya usimamizi wa vyama kwa viongozi mara baada ya uchaguzi kufanyika, kwa kuzingatia kifungu cha 134 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 aya ya 13 ya Jedwali la Pili la Maadili ya Viongozi;

b) Kuhakikisha wanachama, wajumbe wa Bodi na Watendaji wanapata elimu ya ushirika mara kwa mara;

c) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa mpango wa elimu na mafunzo;

d) Kuwa Mwenyekiti wa kamati za elimu ya ushirika kitaifa na mikoa;

e) Kuhakikisha vyama vinatenga tengo la lazima la elimu na mafunzo;

f) Kuhakikisha kuwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika wanapata elimu stahiki, weledi, waaminifu na waadilifu;

g) Kushirikiana na Wadau wengine kutoa elimu ya ushirika kwa umma;

h) kufanya uchambuzi/upembuzi wa mahitaji ya mafunzo kwa kushirikiana na Wadau wengine;

i) Kusimamia watoa huduma ya elimu na mafunzo kwa vyama vya ushirika kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha hususan kwa Vyama vya Ushirika wa Kifedha;

j) Kuhakikisha elimu ya fedha inatolewa kwa Vyama Vya Ushirika wa kifedha kwa kuzingatia Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha na Kanuni zake;

k) Kutafuta rasilimali fedha kwa kushirikiana na wadau mbalimbali

kwa ajili ya kupata wafadhili wa elimu na mafunzo kwa vyama vya ushirika; na

l) Kukusanya taarifa za Elimu na Mafunzo kutoka kwa vyama na wadau mbalimbali;

## 6.2 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU)

a) Kuandaa mitaala ya elimu na mafunzo kwa vyama vya ushirika, wadau wa ushirika na jamii kwa ujumla kulingana na mahitaji;

b) Kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu;

c) Kuendesha programu ya elimu ya masafa kwa wanachama, watendaji, viongozi na wadau wa ushirika;

d) Kushirikiana na TCDC na wadau wengine katika kufanya upembuzi wa mahitaji ya mafunzo;

e) Kuwa Katibu wa kamati za elimu ya ushirika kitaifa na mikoa;

f) Kushirikiana na TCDC na Wadau mbalimbali wa maendeleo ya Ushirika katika kuwajengea uwezo wadau wa Ushirika juu ya matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika juu ya Maendeleo ya Ushirika nchini;

g) Kutoa elimu kwa watoa huduma kuhusu elimu ya ushirika na kutoa mapendekezo kwa Mrajis endapo wanastahili kutoa elimu kwa vyama vya ushirika;

h) Kushirikiana na TCDC kuratibu na kuendesha mafunzo kwa wadau wa ushirika;

i) Kushirikiana na wadau wengine kuandika miradi ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya elimu na mafunzo;

j) Kushirikiana na TCDC na Wadau kutoa elimu ya ushirika kwa umma; na Kuzijengea uwezo kamati za elimu na mafunzo za Mikoa na Taifa ili ziwe na uwezo katika kudhibiti ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa kwenye Vyama vya Ushirika.

## 6.3 Majukumu ya Wadau wengine (TFC & SCCULT)

a) Kushirikiana na TCDC kufanya uchambuzi/upembuzi wa mahitaji ya mafunzo;

b) Kushirikiana na TCDC kuendesha mafunzo kwa wanachama kulingana na mahitaji/ fursa/ miongozo na mpango wa mafunzo kwenye vyama;

c) Kuwasilisha taarifa na mpango wa mafunzo kwa TCDC na kamati ya mafunzo ya Mkoa na Taifa;

d) Kuwasilisha TCDC taarifa ya mafunzo yaliyotolewa kwenye Vyama Vya Ushirika ;

e) Kushirikiana na wadau wengine kuandika miradi ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya elimu na mafunzo; na

f) Kushirikiana na TCDC na wadau wengine wa maendeleo ya ushirika kutoa elimu ya ushirika kwa umma.

## 6.4 Vyama vya Ushirika

Ili vyama viweze kutoa elimu kwa wanachama, viongozi na watendaji, vinapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

a) Kuandaa mpango wa mafunzo kwa ajili ya kuainisha viongozi, watendaji na wanachama watakaoshiriki mafunzo ya mwaka husika.

b) Kutenga tengo kwa ajili ya elimu na mafunzo kwa wanachama, viongozi, watendaji na jamii na kuhakikisha kuwa mpango wa elimu

unatekelezwa kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Vyama vya ushirika, Kanuni, Miongozo na Nyaraka za Mrajis;

c) Kuhakikisha wanachama, wajumbe na watendaji wanapata elimu sahihi kwa kuzingatia mahitaji ya Chama; na

d) Kuandaa taarifa ya mafunzo na kuiwasilisha kwa wasimamizi wa Chama

## SEHEMU YA SABA

## 7.0 UTOAJI WA ELIMU NA MAFUNZO

Mwongozo unaweka utaratibu wa utoaji wa elimu na mafunzo kwa watoa huduma wote wa elimu, ambapo watoa huduma husika watapaswa kuandaa mpango wa elimu wa mwaka na kuuwasilisha kwenye Kamati za elimu na Mafunzo kwa lengo la kujadiliwa na kuidhinishwa na Mrajis. Mara baada ya kuidhinishwa kwa mpango huo, mtoa huduma atatakiwa kuandaa utaratibu wa kutoa mafunzo hayo kwa Vyama vya Ushirika kulingana na mpango kazi wake.

### 7.1 Kamati ya Kitaifa ya Elimu na Mafunzo

Kamati hii itakuwa na wajumbe kutoka katika Taasisi zinazosimamia, kusaidia na kuendeleza ushirika nchini. Taasisi hizi ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) na Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo ( SCCULT). Wajumbe wa Kamati hii watakuwa ni maafisa walio katika ngazi za maamuzi na watateuliwa na wakuu wa taasisi hizo. Aidha, Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa Tume ya

Maendeleo ya Ushirika na Katibu atakuwa ni Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

## 7.2 Majukumu ya Kamati ya Kitaifa ya Elimu na Mafunzo

i. Kushiriki katika kuandaa miongozo na taratibu mbalimbali kwa ajili usimamizi wa masuala la elimu na mafunzo katika vyama vya ushirika;

ii. Kutayarisha kanzi data ya wahusika wote waliopata mafunzo na ambao bado hawajapata mafunzo

iii. Kujenga uelewa wa pamoja kwa wadau wakuu wa elimu ya ushirika;

iv. Kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo Kitaifa;

v. Kupokea na kujadili taarifa za elimu na mafunzo ya ushirika kutoka kwenye kamati za elimu za mikoa na kuzifanyia uchambuzi na kutolea maelekezo kadiri itakavyoonekana inafaa;

vi. Kuweka utaratibu wa kutambua umahiri wa watoa huduma ya elimu na mafunzo; na

vii. Kubuni vyanzo vya fedha (Fund raising) kwa ajili ya utoaji elimu na mafunzo.

## 7.3 Kamati za Elimu na Mafunzo ya Ushirika za Mikoa

Kamati za Elimu na Mafunzo za Mikoa zitakuwa ni vyombo mahsusi katika kuratibu shughuli zinazohusiana na elimu na mafunzo katika Mikoa. Kamati hizi zitahakikisha kunakuwa na takwimu sahihi za elimu na mafunzo yanayofanyika Mikoani na Wilayani kwa kuzingatia mahitaji ya walengwa na viwango vya ubora.

### 7.3.1 Wajumbe wa Kamati za Mikoa

Kamati ya Elimu ya Ushirika ya Mkoa itajumuisha Mrajis Msaidizi, Mratibu wa Mafunzo wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) katika Mkoa husika, Maafisa Ushirika wa Wilaya, Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) katika Ofisi za Mikoa au Kanda, Wajumbe kutoka vyama vikuu vya ushirika na miradi ya pamoja vilivyopo Mkoani. Mrajis Msaidizi atakuwa ndiye Mwenyekiti; Mjumbe kutoka MoCU atakuwa ndiye Katibu wa Kamati; na Wajumbe wengine watapangiwa majukumu kadiri itakavyohitajika.

### 7.3.2 Majukumu ya Kamati za Mikoa

i. Kubaini mahitaji ya mafunzo katika Vyama vya Ushirika;
ii. Kuratibu jitihada za wadau mbalimbali zenye kuwezesha elimu na mafunzo ya ushirika katika Mkoa husika;
iii. Kutayarisha mpango wa Elimu na Mafunzo ya ushirika katika Mkoa kwa ajili ya Wanachama, Viongozi na Watendaji katika Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Mpango wa Kitaifa;
iv. Kuhakikisha kuwa rasilimali kwa ajili ya Elimu na mafunzo katika Vyama vya Ushirika zinapatikana na zinatumika kama ilivyokusudiwa;
v. Kusimamia na kufuatilia huduma zinazotolewa na Watoa huduma ya mafunzo katika mikoa husika;
vi. Kutayarisha kanzi data ya wahusika wote waliopata mafunzo na ambao bado hawajapata mafunzo;
vii. Kutayarisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na elimu na mafunzo ya ushirika na kuziwasilisha kwa Mrajis na kwenye kamati ya Taifa ya elimu na mafunzo ya ushirika;

viii. Kuandaa na kuratibu mafunzo katika Vyama vya Ushirika kulingana na utaratibu uliowekwa;

ix. Kufanya ufuatiliaji na tathmini pamoja na udhibiti wa ubora wa elimu na mafunzo ya ushirika katika mkoa, na

x. Kutekeleza majukumu mengine yote yanayohusiana na Elimu na Mafunzo ya ushirika kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa.

## SEHEMU YA NANE

## 8.0 MBINU ZA KUTOA ELIMU NA MAFUNZO

Ili kuwezesha Elimu na Mafunzo kutolewa ipasavyo, mwezeshaji anatakiwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

i. Vipeperushi;
ii. Mihadhara na Mikutano;
iii. Bungua Bongo;
iv. Majadiliano kwenye vikundi;
v. Kisa Mkasa;
vi. Ziara za mafunzo;
vii. Mitandao ya Kijamii;
viii. Elimu ya masafa inayotolewa na wadau mbalimbali,
ix. Vyombo vya Habari.

## SEHEMU YA TISA

## 9.0 UFUATILIAJI, TATHMINI NA URATIBU

Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na wadau, itafanya Ufuatiliaji, tathmini na uratibu ili kuhakikisha elimu na mafunzo yanatolewa kikamilifu katika Vyama vya Ushirika. Hatua za ufuatiliaji zitahusisha ukusanyaji wa taarifa muhimu juu ya utekelezaji wa mpango wa mafunzo, kutathmini na kupima ufanisi wa mafunzo.

Taarifa ya kila robo, nusu na ya mwaka juu ya elimu na mafunzo itakuwa inatolewa na kila chama cha ushirika kupitia kwa Afisa Ushirika wa eneo husika. Tathmini hii itasaidia kufanya maboresho katika mafunzo yatakayofuata. Aidha, Afisa Ushirika/Mrajis Msaidizi wa eneo husika atapaswa kuwasilisha taarifa ya Elimu na Mafunzo kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## 10.0 HITIMISHO

Mwongozo huu ukitumika vyema utasaidia kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo yanayotolewa yataviwezesha vyama kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kuwa endelevu katika mazingira ya uchumi wa Soko huru.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na wadau itaendelea kufuatilia na kuhakikisha kuwa elimu ya ushirika inaingizwa kwenye mitaala na mifumo ya Elimu ya Taifa. Ni mategemeo ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuwa wadau wote wa ushirika watazingatia mwongozo huu katika utoaji wa elimu katika Vyama vya Ushirika nchini.